



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE



Simu Na: +255 (026) 2740016
Nukushi: +255 026 2740103
BaruaPepe: ded@makete.go.tz
Tovuti: <http://www.maketedc.go.tz>
Unapojibu tafadhali taja;

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri Wilaya ya Makete,
4 Barabara ya Bomani,
59582 MAKETE, NJOMBE,
S.L.P 6, MAKETE

Kumb. Na.EB.22/124/01/65

22/03/2023

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ifuatayo: -

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III - NAFASI 1

Sifa za muombaji

1. Awe na Cheti cha Kuhitimu na kufaulu kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI)
2. Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada katika moja ya fani zifuatazo; Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Kijiji
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika kijiji na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa Njaa, Umasikini na Kuongeza Uzalishaji mali.

- vii. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaaluma katika Kijiji
- viii. Kusimamia, Kukusanya na Kuhifadhi Kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- x. Kupokea, Kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za kijiji
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MSHAHARA.


Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kina ngazi ya Mshahara wa TGS B kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yeyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Makete.
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 na usiozidi 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Details CV) namba za simu na anwani sahihi.
4. Maombi yote ya mwombaji yaambatane na nakala ya Vyeti vya Taaluma, vyeti vya kidato cha (IV au IV), Cheti cha Kuzaliwa na picha mbili (2) za passport size za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.
5. Testimonials na "Provisional statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA**
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyako vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NACTE) na taarifa ya Uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.
7. Siku ya Usaili kila mwombaji afike na Vyeti halisi (Original) vya Elimu, Taaluma, Kuzaliwa na Kitambulisho.
8. Waombaji waliostaafishwa au kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
9. Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kughushi ni kosa kisheria na wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.
10. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 11/04/2023 saa 9:30 alasiri.
11. Maombi yaambatanishwe na nakala ya kitambulisho cha **NIDA**.

12. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa Anwani ya :-

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Makete,
S.L.P 6
MAKETE


Apollo E. Laizer
Kaimu-Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
MAKETE

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MAKETE

Nakala:

Katibu wa Tume,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
DODOMA.

Tovuti ya Halmashauri

www.maketedc.go.tz

Meneja Redio Kitulo FM

Mbao za Matangazo